



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**



Simu Na. 023 293 7043  
Nukushi: 0737-187605  
Barua Pepe: ded@liwaledc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P 23,  
**LIWALE.**

**Unapojibu tafadhali taja;**

Kumb. Na. LW/DC/L.20/10 VOL. X/28

03/03/2023

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale anakaribisha maombi ya Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za Kazi za Mteknolojia Dawa Msaidizi kama ifuatavyo;

### **1. MTEKNOLOJIA DAWA MSAIDIZI – NAFASI TATU (3)**

#### **A. KAZI NA MAJUKUMU YA MTEKNOLOJIA DAWA MSAIDIZI.**

- i. Kuainisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi.
- ii. Kuuza dawa na vifaa tiba kwa wateja/wagonjwa.
- iii. Kuhifadhi dawa na vifaa tiba.
- iv. Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa.
- v. Kukagua dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi katika Duka la Dawa la Hospitali.
- vi. Kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa.
- vii. Kushiriki kazi za kamati ya usimamizi wa Duka la Dawa la Hospitali.
- viii. Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba.
- ix. Kufanya uchunguzi wa ubora wa dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi.
- x. Kufanya kaguzi mbalimbali katika sehemu zinazohifadhi dawa.
- xi. Kusimamia utendaji wa kazi watumishi walio chini yake.
- xii. Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba pamoja na taarifa za mwezi za Duka la Dawa.
- xiii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

#### **B. SIFA ZA MWOMBAJI.**

Awe na Astashahada/Cheti (Certificate) katika fani ya Uteknolojia dawa wasaidizi kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Baraza la Wafamasia.

#### **C. MSHAHARA**

Kwa kuzingatia waraka wa Serikali mshahara ni TGHS A.

## **MASHARTI YA KAZI/WAOMBAJI KWA UJUMLA**

- i. Awe raia wa Tanzania.
- ii. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- iii. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- iv. Awe na Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIN).
- v. Nafasi ya Kazi inayoombwa iandikwe katika kichwa cha habari cha barua.
- vi. Waombaji waambatishe maelezo binafsi **yanayojitosheleza (a detailed C.V)** yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya **wadhamini (referees) watatu** wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- vii. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma na mafunzo kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali:
  - Cheti cha mthani wa Kidato cha IV
  - Cheti cha mafunzo (professional).
  - Cheti cha kuzaliwa.
  - Picha Moja "Passport Size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
  - Usajili kamili (Full Registration) au Leseni hai ya kufanya kazi ya taaluma husika.
- viii. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali au Mwajiriwa wa Hospitali za Mashirika ya Dini ambaye mshahara wake unalipwa na Serikali.
- ix. Waombaji walioajiriwa kwa mkataba wa ajira kutoka kwa Wadau wa Maendeleo katika Sekta ya Afya wanatakiwa kuambatisha nakala za mkataba na barua za uthibitisho kutoka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri husika.
- x. Awe hajawahi kufukuzwa, kuacha kazi au kustaafishwa katika Utumishi wa Umma.
- xi. "Testimonials", "Provisional results", "Statement of results", hati za matokeo za kidato cha IV na VI (form IV and form Vi result slips) HAVITAKUBALIWA.
- xii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi zitapelekea wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.
- xiii. **Nakala za vyeti vyote viwe vimethibitishwa (Certified copies).**
- xiv. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **16/03/2023 saa 9:30** alasiri.
- xv. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo.

*Barua zote zitumwe kwa anwani iliyopo hapa chini.*

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S.L.P 23,  
LIWALE.**

Aidha, barua za maombi zinaweza kuwasilishwa moja kwa moja katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale.

Limetolewa na;

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
LIWALE**